



NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI MIRADI YA TATHIMINI TA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM)

Ibara ya 17 ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imeainisha madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya mazingira. Pamoja na masuala mengine Baraza limepewa majukumu ya kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Jukumu hili linahusisha kuratibu, kufanya mapitio ya taarifa za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake. Aidha, Ibara ya 18 (2) ya Sheria ya Mazingira inatoa mchanganuo mpana wa majukumu ya Baraza ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki na ukaguzi wa mazingira (Environmental Audit) na kufanya tathmini ambazo zitasaidia katika kuhifadhi na kusimamia mazingira.

Katika kuboresha mifumo yake ya mapitio ya taarifa za tathmini na kaguzi za athari za mazingira, Baraza limeimarisha miundo mbinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kulingana na matakwa ya Mfumo wa Serikali Mtandao (e-Government). Hivyo, mnafahamishwa ya kuwa Baraza limekamilisha mfumo wa kielektroniki wa kusajili Miradi ya Tathmini za Mazingira na Ukaguzi (*Online Registration and Tracking System*). Pia taratibu za serikali za kuukagua mfumo huu katika masuala ya usalama zimekamilika. Mfumo huu utawawezesha wawekezaji kusajili miradi yao na kufuatilia mchakato wa Hati ya Mazingira kwenye mtandao (*Online*).

Mfumo huu utatumiwa na makundi husika kama ifuatavyo:

- i. Waandaaji wa Miradi kusajili mradi;
- ii. Watumishi wa Baraza kupokea na kufanyia kazi maombi yanayowasilishwa ya TAM; na
- iii. Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) watatumia mfumo huu kufanyia kazi maombi ya TAM kabla ya Waziri kuidhinisha utekelezaji wa miradi.

Mfumo huu ni mahususi katika jitihada zinazofanywa na Baraza za kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha mazingira bora na wezeshi kwa wawekezaji hususan walio na lengo la kuanzisha shughuli za maendeleo. Hivyo

basi, mfumo huu unakusudiwa kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi na pia kulisaidia Baraza katika kuwa na kumbukumbu za uhakika katika masuala yanayohusu miradi na usimamizi wa mazingira. Aidha, mfumo huu utasaidia wawekezaji kufuatilia kwa karibu mchakato wa Hati ya Mazingira. Aidha, malipo yote ikiwa ni pamoja na gharama za usajili na gharama za mapitio ya miradi yanafanyika kwa mfumo wa malipo wa serkali wa kielektroniki ikiwa ni pamoja na kupata hati ya madai (invoice) na kumbukumbu namba ya malipo (control number).

Mfumo huu unapatikana kwenye tovuti za Baraza kutokana na kundi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

- i. **Waandaaji wa Miradi (eia.nemc.or.tz);**
- ii. **Watumishi wa Baraza (pms.nemc.or.tz); na**
- iii. **Watumishi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (vpo.nemc.or.tz).**

Kwa misingi hiyo na kuufanya mfumo huo utumike, taasisi zote nchini, wawekezaji, wataalam elekezi, wananchi na wadau wote wa mazingira mnataarifiwa kuwa mfumo huo umeanza kutumika na utakuwa kwenye kipindi cha majaribio hadi Oktoba 30 ambapo usajili wa miradi yote utafanyika kwa namna zote mbili ikiwa ni pamoja na kutumia mfumo wa awali wa kusajili miradi kwa kuwasilisha taarifa (*hard copies*) masijala (*Registry*) na vile vile kwenye mtandao kwa kutumia tovuti iliyoainishwa hapo juu. Baada ya hapo usajili wa miradi yote utakuwa kwa mfumo wa kielektroniki pekee.

Kwa Taarifa zaidi tembelea tovuti ya Baraza (nemc.or.tz) au tembelea Ofisi za Makao Makuu ya Baraza zilizopo katika Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent, Mikocheni kabla ya Tarehe 15 Juni 2019 au katika ofisi za kanda za Baraza zilizopo Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Mtwara.

Limetolewa na:

***MKURUGENZI MKUU,
BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)***

Limesambazwa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Viwanja Na. 28, 29 &30-35, Mtaa wa Regent, S.L.P 63154, Dar es Salaam. Simu ya mezani: +255 22 2774889, moja kwa moja: +255 22 2774852 simu za mkononi: 0713 608930/0692108566 Fax: +255 22 2774901, Barua pepe: dg@nemc.or.tz